

STORY OF THE MONTH

WELCOMING THE NEW MANAGER: A CATALYST FOR POSITIVE CHANGE

Fountain Gate Foundation is excited to welcome Mr. Eliasa Abdallah Hussein as the new Manager marking the beginning of an important phase of growth and transformation. His strong background in management and community development brings fresh vision, renewed energy and a results-driven approach to the Foundation.

Since his arrival, Mr. Eliasa has shown commitment to strengthening systems, improving teamwork and driving innovation. His leadership has sparked positive momentum and encouraged staff to embrace change while aligning with the Foundation's mission of empowering children, youth and communities.

The Foundation Fountain Gate looks forward to a new era of improved efficiency, transparency and impact under his guidance.



HIGHLIGHT FROM NOVEMBER

FOUNTAIN DODOMA PRE AND PRIMARY SCHOOL SHINES IN 2025 EXAMINATIONS

PSLE 2025 EXAMINATION RESULTS

FOUNTAIN DODOMA PRIMARY SCHOOL - PS0302129

WALIOFANYA MTIHANI : 190

WASTANI WA SHULE : 287.7000 **DARAJA A (BORA)**

MADARAJA YA UFAULU WA UJUMLA

JINSI	A	B	C	D	E
WASICHANA	80	0	0	0	0
WAVULANA	110	0	0	0	0
JUMLA	190	0	0	0	0

Fountain Dodoma Pre and Primary School has once again demonstrated outstanding academic excellence after securing 1st position in the Dodoma Region and an impressive 30th position nationally in the 2025 examinations.

This remarkable achievement reflects the school's commitment to high quality education, effective teaching strategies, and a supportive learning environment that empowers every child to succeed. Notably, all candidates who sat for the exam achieved Grade A, marking a rare and exceptional performance that highlights both student dedication and strong institutional support.

The school management has expressed profound appreciation to teachers, parents, and guardians for their continued cooperation, and congratulated the candidates for representing the school with excellence.

Fountain Dodoma Pre and Primary School remains committed to nurturing confident, disciplined, and high performing learners who are prepared to excel in every stage of their academic journey.

UPCOMING EVENTS

FOUNTAIN GATE FOUNDATION CELEBRATES MILESTONE ACHIEVEMENTS OF SPONSORED STUDENTS

The Fountain Gate Foundation continues to make remarkable strides in transforming lives through access to quality education. In line with its mission to nurture dreams and empower young people, the Foundation is proud to celebrate the success of four students who are set to graduate in 2025 under its sponsorship program.

This year's milestone is particularly special, as it highlights the Foundation's impact across different educational levels. Two students will be completing their primary education at the Standard Seven level, while nine others will be graduating from secondary school at Form Four. All four students have been fully supported by the Foundation, reflecting its unwavering commitment to ensuring that every child, regardless of background, has the opportunity to pursue excellence in education.

These achievements not only mark personal triumphs for the students but also showcase the Foundation's vision in action providing a solid foundation for children and youth to realize their potential and achieve their dreams. By bridging the gap between talent and opportunity, Fountain Gate Foundation continues to serve as a beacon of hope for families and communities, proving that education is the most powerful tool to change lives.

www.fountaingateacademy.com
www.fountaingatef.or.tz
www.fountaingatesports.co.tz

SPORT ACADEMY UPDATES

FOUNTAIN GATE SCHOOLS SET FOR STRONG REPRESENTATION AT THE CHIPUKIZI TOURNAMENT IN ARUSHA

Fountain Gate Schools are gearing up to participate in this year's Chipukizi Tournament, scheduled to take place in Arusha. The tournament, which gathers young football talent from across the country, offers an important platform for students to display their skill, discipline, and passion for the game.

Fountain Gate will be represented by four football teams drawn from its various campuses. The teams have been undergoing intensive training, guided by experienced coaches who are committed to developing both talent and character among young players.

Fountain Gate Schools extend their best wishes to all participating players and look forward to a successful and memorable football tournament in Arusha.



KISA CHA MWEZI

KUMKARIBISHA MENEJA MPYA: CHACHU YA MABADILIKO CHANYA

Fountain Gate Foundation inafuraha kumkaribisha Bw. Eliasa Abdallah Hussein kama Meneja Mpya, tukio linaloashiria mwanzo wa hatua muhimu ya ukuaji na mabadiliko ndani ya taasisi. Uzoefu wake katika usimamizi na maendeleo ya jamii unaleta mtazamo mpya, ari mpya na uongozi unaolenga matokeo.

Tangu kuwasili kwake, Bw. Eliasa ameonyesha dhamira ya kuimarisha mifumo ya kazi, kuboresha ushirikiano wa timu na kuendesha ubunifu. Uongozi wake umeleta mwamko chanya na kuhamasisha watumishi kukumbatia mabadiliko sambamba na dhamira ya Foundation ya kuwawezesha watoto, vijana na jamii.

Fountain Gate Foundation ina matumaini kwamba chini ya uongozi wake, kutakuwepo na ufanisi zaidi, uwazi na matokeo yenye athari kubwa kwa jamii.



MATUKIO MUHIMU MWEZI WA NANE

FOUNTAIN DODOMA PRE AND PRIMARY YANG'ARA KATIKA MITIHANI YA 2025

PSLE 2025 EXAMINATION RESULTS

FOUNTAIN DODOMA PRIMARY SCHOOL - PS0302129

WALIOFANYA MTIHANI : 190

WASTANI WA SHULE : 287.7000 **DARAJA A (BORA)**

MADARAJA YA UFAULU WA UJUMLA

JINSI	A	B	C	D	E
WASICHANA	80	0	0	0	0
WAVULANA	110	0	0	0	0
JUMLA	190	0	0	0	0

Shule ya Fountain Dodoma Pre and Primary Yang'ara Katika Mitihani ya 2025 Shule ya Fountain Dodoma Pre and Primary imeendelea kung'ara kitaaluma baada ya kushika nafasi ya 1 kimkoa (Dodoma) na nafasi ya 30 kitaifa katika matokeo ya mtihani wa mwaka 2025. Haya ni mafanikio makubwa yanayoonesha dhamira ya shule katika kutoa elimu bora, mbinu madhubuti za ufundishaji, na mazingira rafiki yanayowawezesha wanafunzi kufikia viwango vya juu vya ufaulu.

Kwa mafanikio ya kipekee, wanafunzi wote waliofanya mtihani wamepata Daraja A, jambo linaloonesha juhudi za wanafunzi pamoja na mwongozo na ushirikiano mkubwa kutoka kwa walimu na uongozi wa shule.

Uongozi wa shule umeeleza shukrani za dhati kwa walimu, wazazi na walezi kwa ushirikiano wao, sambamba na kuwapongeza wanafunzi kwa kuiletea heshima shule kupitia matokeo bora.

Fountain Dodoma Pre and Primary School inaendelea kujikita katika kulea wanafunzi wenye uwezo, nidhamu, na uelewa wa juu, tayari kwa mafanikio katika hatua zote za safari yao ya elimu.

MATUKIO YAJAYO

FOUNTAIN GATE FOUNDATION YASHEREHEKEA MAFANIKIO YA WANAFUNZI WANAODHAMINIWA

Shirika la Fountain Gate Foundation linaendelea kufanya maendeleo makubwa katika kubadilisha maisha kupitia upatikanaji wa elimu bora. Kwa kuzingatia dhamira yake ya kulea ndoto na kuwawezesha vijana, Fountain Gate Foundation inajivunia kusherehekea mafanikio ya wanafunzi kumi na moja watakaohitimu masomo mwaka 2025 chini ya mpango wake wa ufadhili.

Tukio la mwaka huu ni la kipekee kwani linaonyesha kwa namna ya pekee athari chanya za Fountain Gate Foundation katika ngazi tofauti za elimu. Wanafunzi wawili watamaliza elimu ya msingi, huku wengine tisa wakihitimu elimu ya sekondari. Wote hawa wamekuwa wakihudumiwa kwa ukamilifu na Fountain Gate Foundation, jambo linalodhihirisha dhamira thabiti ya kuhakikisha kila mtoto, bila kujali mazingira yake, anapata nafasi ya kupata elimu ubora.

Mafanikio haya siyo tu ushindi binafsi kwa wanafunzi husika, bali pia ni kielelezo cha maono ya Fountain Gate Foundation katika utekelezaji, ikiwapatia watoto na vijana msingi imara wa kutimiza ndoto zao na kufikia malengo yao. Kwa kujenga daraja kati ya kipaji na fursa, Fountain Gate Foundation inaendelea kuwa taa ya matumaini kwa familia na jamii, ikithibitisha kwamba elimu ndiyo nyenzo yenye nguvu zaidi ya kubadilisha maisha.

www.fountaingateacademy.com
www.fountaingatef.or.tz
www.fountaingatesports.co.tz

Tufuatilie Kupitia:



YANAYOJIRI KITUO CHA MICHEZO FOUNTAIN GATE

SHULE ZA FOUNTAIN GATE ZAJIANDAA KUSHIRIKI KWA UZITO KATIKA MASHINDANO YA CHIPUKIZI JIJINI ARUSHA

Shule za Fountain Gate zinajiandaa kushiriki katika Mashindano ya Chipukizi yatakayofanyika jijini Arusha mwaka huu. Mashindano haya, ambayo hukusanya vipaji vya soka vya vijana kutoka maeneo mbalimbali nchini, ni jukwaa muhimu kwa wanafunzi kuonyesha uwezo wao, nidhamu na mapenzi ya mchezo wa mpira wa miguu.

Fountain Gate itawakilishwa na timu nne za mpira wa miguu kutoka kampasi zake mbalimbali. Timu hizi zimekuwa zikifanya mazoezi makali chini ya usimamizi wa makocha wenye uzoefu mkubwa katika kukuza vipaji na tabia bora kwa wachezaji chipukizi.

Shule za Fountain Gate zinawatakia mafanikio mema wachezaji wote watakaoshiriki na zinatarajia mashindano yenye ushindani na kumbukumbu njema jijini Arusha.

